



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA



ISO 9001:2015 Certified

Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAZIWA MBADALA YA WATOTO (BREAST MILK
SUBSTITUTE) AINA YA **INFACARE**

Dar es Salaam, 15 Mei, 2024

Mnamo tarehe 10 Mei 2024, Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA) ilitoa taarifa kwa umma juu ya uwepo wa maziwa mbadala ya watoto aina ya **Infacare 1, 2 na 3** yaliyoandikwa **“Not for Resale in Tanzania”** ambayo yaliingizwa Zanzibar pasipo kufuata utaratibu na hivyo kusitishwa matumizi na kuondolewa katika soko.

TBS inapenda kuutaarifu umma kuwa imesajili bidhaa za **Infacare 1, 2 na 3** zinazozalishwa na kiwanda cha **Sanulac Nutritionals South Africa (Pty) Ltd.** cha Afrika Kusini baada ya kuhakiki ubora na usalama wake. Taarifa za kwenye bidhaa za **Infacare** zilizosajiliwa zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa pamoja kwa mujibu wa Kiwango EAS 4-1:2021 na Kanuni za Usajili wa Bidhaa na Uthibitishaji Ubora wa Shehena [The Standards (Imports Registration and Batch Certification) Regulations, 2021].

Bidhaa zilizosajiliwa hazijaandikwa **“Not for Resale in Tanzania”** hivyo wananchi wanaombwa kutoa taarifa kupitia namba **0800110827** endapo watabaini kasoro zozote kwenye taarifa zilizopo kwenye vifungashio vya maziwa mbadala ya watoto.

TBS inatoa rai kwa wananchi wanaponunua aina yoyote ya maziwa mbadala ya watoto kuhakikisha kuwa yameandikwa kwa lugha zote mbili yaani Kiswahili na Kiingereza kwani maziwa yenye lugha hizo yamehakikiwa ubora na usalama wake na yamefuata taratibu za uingizwaji nchini na hivyo yameruhusiwa kuuzwa.

TBS inaendelea kuwakumbusha wafanyabiashara kufuata taratibu za uingizwaji wa bidhaa nchini kwani hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wauzaji, wasambazaji na waingizaji watakaobainika kuvunja taratibu za kisheria.

Imetolewa na:

Gladness H Kaseka
MENEJA UHUSIANO NA MASOKO

TBS MAKAO MAKUU

Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma /
Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/
+255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya
wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA
KATI**

Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 26 2520310

**TBS KANDA YA
ZIWA**

Jengo la NSSF,
Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2505044

**TBS KANDA YA
KASKAZINI**

Jengo la NSSF (Mafao
House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 27 2520143

**TBS KANDA YA
NYANDA ZA JUU
KUSINI**

Jengo la NHIF,
Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na:
+255 25 2502848

**TBS KANDA YA
KUSINI**

Jengo la
MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 23 2334477

**TBS KANDA YA
MAGHARIBI**

Jengo la NSSF (Mafao
House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA,
TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2804023